



Marafiki wapendwa

Tuna tumaini kwamba nyote na familia zenu hamjambo na mu wazima wa afya.

Kama mnavyojua siku ya kimataifa ya familia inasherehekewa kila mwaka siku ya tarehe 15 Mei tangu mwaka 1994. Katika sehemu ya pili ya kijarida hiki tutajaribu kujiandaa kwa ajili ya siku hiyo.

Lakini kwanza tunataka kuwapa ushuhuda wa Bi. Moshi Nyashebo aliyekuwa kwa muda mrefu katika shirika la "Single Unemployed Women" (wanawake wajane na wasio na kazi) lililopo Dar es Salaam. Tunadhani sisi sote tunahitaji kujua kwamba hatuko peke yetu katika mahangaiko dhidi ya umasikini uliozidi kiasi. Raia wengi wanajitoa katika maeneo wanayokaa, wanapofanya kazi na katika mashirika. Wanajitoa kwa njia tofauti na kusikia juu ya uzoefu wao inatupa moyo wote.

Tunawatakia kusoma kwema!

Dear friends,

We hope everything is fine with you and your family and that you are all in good health.

As you know the International Day of Families is celebrated every May 15th since 1994. In the 2nd part of this Newsletter, we will try to prepare ourselves for this day.

But first of all, we would like to share with you the testimony of Mrs Moshi Nyashebo who has, for a long time, been involved in the association "Single Unemployed Women" in Dar es Salaam. We think that all of us need to know that we are not alone in our struggle against extreme poverty. Many citizens are committed in their neighbourhood, their job, some associations... in very different ways and the sharing of experiences is an encouragement for everyone.

Have a good reading !

Bila kujali nitapata nini ...

Nashiriki katika chama kinachosaidia wanawake wajane. Nia yangu ni kuwawezesha hawa wanawake kutenda ili wapate maisha bora zaidi. Wengi hawapendi hali yao ya maisha kwa sababu ya mapato yao madogo ambayo hata hayatoshi kwa mlo mmoja.

Kujitoa kwangu pia ni kwa ajili ya kubadili ujuzi wangu, mawazo na uelewa juu ya maisha ya watu maskini.

Chama changu kinamsaidia mtu mmoja mmoja kwa kuwashirikisha kwenye kikundi kidogo na kuwasaidia na matatizo yao ya kifamilia. Watoto wao wanaenda shuleni? Chumbani kwao watu wa jinsia tofauti wamejaa?... Chama chetu kinatoa ushauri na kuwasaidia wanawake wajane ili waweze kupata sehemu nzuri kuishi pamoja na familia zao.

Without caring about what I will get...

I am involved in an association which helps single women. My aim is to support these women to act in order to have a better life. Many of them are unhappy with their life conditions because of their meagre income which is not even enough for a single meal.

My commitment is also to change myself with regard to knowledge, thinking patterns and in obtaining a better understanding of the life of the poor people.

My association deals with helping individual people by integrating them into a small group, and caring about the problems of their family. Do their children go to school ? Is their room overcrowded by people of the two genders ?... Our association advises and helps single women so that they can get a good place to live with their families. I give counselling to



Natoa ushauri nasaha kwa wale wanaohitaji, nawasaidia wale wanaotaka kuanzisha biashara ya mama lishe kupata mtaji. Nikimsaidia mtu mmoja kupata maisha bora, huyu mtu ataweza kumsaidia mwingine aliye na maisha magumu zaidi. Na wakijiunga kwenye kikundi watakuwa kama jamii moja.

Shughuli zangu binafsi ni kama kawaida: ninalima, nina mashamba kijijini huko mkoa wa Pwani ambapo nalima. Hata hivyo, kwa sababu ya shughuli zangu za kujitolea, nakosa muda wa kufanya shughuli zangu binafsi zinazoongeza mapato yangu. Kuna watu wengi walio na matatizo kila siku, kwa hiyo natumia muda wangu mwingi kuwasaidia. Ni chaguo langu, lakini siku nyingine sina muda wa kutosha kwenda na kufanya shughuli zangu binafsi kwa hiyo inabidi nimwombe mwingine kuzifanya kwa ajili yangu.

Najitoa kwa shughuli hizi kwa sababu najibu wito kutoka kwa Bwana, wito wa kujitoa kwa kuhudumia wengine, bila kujali nitapata nini.

those who are in need, helping them to obtain capital to start a business selling meals. If I help one person to improve their way of life, then this person can help another who has an even harder life. And when they are in a group they become like one community.

My personal business is just normal : I am farming. I have some fields which I cultivate in a village of the Coastal Region. However, because of my voluntary activities, I do not find the time to attend to my own personal activities that will increase my income. There are many people who have constant problems, and so I use most of my time to help them. It is my choice, but sometimes I do not have enough time to go and do my private business and I have to ask someone to go and do it for me.

I am committed in these activities because I answer a call from the Lord, a call to put myself at the service of others, without caring about what I will get.

Tarehe 15 Mei, Siku ya kimataifa ya familia

May 15th, The International Day of the Family

Siku inayokuja ya kimataifa ya familia ambayo ni tarehe 15 Mei itasherehekewa duniani kote na bila shaka hata hapa Tanzania. Mwaka huu mada ya siku hii ni "Mama na familia, changamoto gani katika ulimwengu unaobadilika?" Siku hii ni muhimu pia kwa sababu ni fursa ya kutukumbusha nafasi muhimu inayochukua familia katika kukwamua umasikini unaozidi kiasi. Katika familia wasio na fursa, kinachowapa moyo wazazi na kuwasaidia kupambana na ugumu wa maisha yao na kudhalilishwa siku hadi siku ni matumaini kwamba watoto wao watapata maisha bora kuliko ya kwao. Katika familia hizo watoto wanakua wakijifunza kujivunia wazazi wao na marafiki zao ambao hawakati tamaa katika maisha yao magumu.

Joseph Wresinski, aliyeanzisha Shirika la kimataifa ATD Dunia ya Nne, alizaliwa na kukua katika familia maskini kuzidi kiasi. Alijua kukosa fedha, kuteseka, kudhalilishwa... Katika sehemu inayofuata anatuambia jinsi mama yake alivyowafundisha watoto wake kujivunia.

Next May 15th, the International Day of Families will be celebrated throughout the world, and of course in Tanzania. This year the theme of the day is "Mothers and families, which challenges in a changing world ?" This day is important as well because the occasion serves to remind us of the essential role of the family in overcoming extreme poverty. In the very disadvantaged families, what supports the parents and gives them courage, day after day, to resist the difficulties and humiliations of their life, is the hope they have that their children will have a better future than themselves. In these families, the children grow up learning to be proud of their parents, and their friends, who do not give up in the face of so many challenges in life.

Joseph Wresinski, the founder of the International Movement ATD Fourth World, was born and grew up in an extremely poor family. He knew the lack of money, the sufferings, the humiliations... In the text below; he tells us how his mother taught her children to be proud.

Kwa kweli nilikuwa mtoto mtukutu kabisa katika mazingira yote ya jirani na daima nilikuwa katika matatizo ya kila namna. (...) Jirani zangu hawakupendezwa kabisa na tabia yangu na wakati mwingine nilimsababishia mama yangu matatizo makubwa sana. Mama alihofia sana kuhusu sifa njema ya familia, hivyo watu walimshauri aniweke katika nyumba ya yatima. Kila mtu alipendekeza hivyo. Kisha usiku ule kabla sijaondoka, mama alisema, "Hapana, haiwezekani, wewe si yatima, unaye mama wewe!"

Hakika mama yangu ndiye aliyenisababisha nijihusishe na familia zinazoishi katika wimbi la umaskini. Baba yangu aliondoka nyumbani kwenda kutafuta kazi, hivyo mama yangu alibaki peke yake akiwa na watoto wanne.. hata hivyo tunamshukuru mama kwamba hatukuwa na majonzi ingawa mara kwa mara tulidhalilishwa, lakini mara zote mama alifahamu jinsi ya kutufanya tujisikie vizuri tena. Tunamshukuru kwamba kwa jinsi hiyo tulikuwa na utambulisho, kwamba tulikuwa watu fulani katika mazingira ya jirani.

Hata katika hali ya ufukara wake, mama daima kwa namna moja ama nyingine alipata msaada kwa sababu alilinda heshima yake na kujivunia hali yake. Daima alitufundisha kuwa na fahari katika hali yetu. Endapo mtu yeyote alionesha hali ya kutudharau, mama alimkemea akisema, "kamwe sikubaliani na hilo." Kwa jinsi hiyo, watu walituheshimu.

Katika sehemu ya pili, Joseph Wresinski anawaambia familia maskini zaidi kuwa na fahari ndani yao kwa sababu ya moyo wa mama na baba walionao.

Fahari. Kuwa na fahari katika nafsi ni jambo la muhimu. Familia lazima zione fahari. Kina mama wanao moyo na lazima wajue hivyo.

I was really the worst child of the neighbourhood and got into all kinds of trouble. (...) The people in my neighbourhood were not too happy with my behaviour and sometimes it was hard on my mother. She was afraid for the family's reputation and so people told her I should be put in an orphanage. Everybody got involved. Then the night before I was to leave, my mother said : "No, you're not an orphan. You have a mother".

It was because of my mother that I got involved with very poor families. My father had left to find work, so my mother was on her own, with four children. But, thanks to her, we weren't unhappy. We were often humiliated, but my mother always knew how to make us feel better again. And thanks to her, we had an identity, we were someone in the neighbourhood. (...)

My mother was always helped in one way or another, in spite of her poverty, she kept her honour and her pride. She taught us to be proud. When someone wasn't respectful with us she said, "No, I won't accept that". She made people respect us.

In this 2nd text, Joseph Wresinski calls the poorest families to find pride in themselves, because of the courage of the mothers and the fathers.

Pride, to have pride in ourselves, is the important thing. The families must be proud. The mothers are courageous and they must



Michoro ya / Drawing by Kitwana Kombo

Lazima wawe na fahari kwa jinsi wanavyolea watoto wao wakati kipato chao ni finyu. Kina baba hawana budi wajivune kwa sababu hata katika hali ya kutokuwa na fedha, hata katika hali ambayo matumbo yao huwa matupu tena wakivaa nguo zisizo na maana, lakini bado wanakwenda kazini. Ndiyo. Tena kwa fahari.

Kwa fahari hii watadai kila kitu: watadai elimu, haki ya elimu kwa watoto wao, hususan wakizingatia zaidi wale walio wadogo zaidi. Kwa sababu ni kuanzia katika umri mdogo ndipo watoto hujifunza kujivunia mazingira yao halisi. Wanapaswa wafunzwe kupenda asili yao, kama jinsi wanavyojipenda wao wenyewe. Lazima wafundishwe kuwapenda rafiki zao, watu waliokua pamoja, ili kwamba kamwe wasiwasahau na kuachana na watu wa kwao.

Familia ni kama ngao inayozuia umaskini uliozidi kiasi kuharibu ubinadamu. Kwa sababu hiyo ni muhimu sana kulinda na kusaidia familia. Kusherehekea Siku ya kimataifa ya familia inaweza kuwa njia moja kuwawezesha wazazi kujivunia kulea watoto wao licha ya maisha magumu. Na njia ya kuwawezesha watoto kujivunia moyo wa wazazi wao kila siku pia.

know that. They must be proud of the way they bring up their children with so few resources. The fathers must be proud because, in spite of an empty stomach and without the proper clothes, they still go to work. Yes, pride.

With this pride they will demand everything: they will demand the right to education for their children, and especially that attention be paid to the youngest. Because from the earliest age, the children must learn to be proud of their background. They must learn to love where they come from, their father and their mother, as much as themselves. They must be taught to love their friends, the people with whom they grew up, so that they will never forget and reject their own people.

Family is like a shield which prevents extreme poverty from destroying the human being. That is for why it is so important to protect and support families. To celebrate the International Day of Families can be a way to allow the parents to be proud of how they take care of their children in spite of their tough life. And a way to allow the children to be proud of the daily courage of their parents as well.

Sehemu hizi mbili zinatoka katika kitabu "Maisha Yake, Maisha Yetu", iliyotolewa mwaka jana katika lugha ya Kiswahili, rafiki yetu Constantine Saasita Munema alikitafsiri.

Ukipenda kupata kitabu hiki (kinapatikana katika Kiswahili na Kiingereza), utuambie tu na tutafurahi kukutumia¹.

Tuambie jinsi utakavyosherehekea Siku hii ya kimataifa ya familia!

*Timu yenu ya ATD Dunia ya Nne
Dar es Salaam*

The two texts above are excerpts from the booklet "His Life, Our Lives", which was published last year in Swahili language, in a translation made by our friend Constantine Saasita Munema.

If you are interested to receive this booklet (available in Swahili and in English), just tell us and we will be happy to send it to you¹.

Tell us how you are going to celebrate this International Day of Families !

*Your ATD Fourth World Team
in Dar es Salaam*

¹Tutashukuru ukiweza kuchangia gharama za uchapaji na kutuma (Tshs 1000).

¹Thank you if you can contribute to the printing and postal expenses (Tsh 1000).